

1. MFUMO WA USAJILI WA WATOA HUDUMA YA MSAADA WA KISHERIA (Legal Aid Database System)

Mfumo huu ni mahsusi kwa ajili ya;-

Kumwezesha mtuma maombi ya kazi ya utoaji wa huduma ya Msaada wa Kisheria, kutuma maombi yake kwa Msajili kwa njia ya kielektroniki na kupata mrejesho ndani ya muda mfupi

Kumwezesha mwanachi anayehitaji huduma ya msaada wa kisheria kufahamu watoa huduma za msaada wa kisheria walio karibu yake na kufanya mawasiliano kwa urahisi Zaidi.

Wananchi na watoa huduma za Msaada wa Kisheria wanaweza kuufikia mfumo huu kwa kupitia anuani ya; <https://legalaidsheria.go.tz/> na kufuata maelekezo.

2. MFUMO WA KUPOKEA MALALAMIKO (Complaints Handling System)

Ni mfumo wa kupokea malalamiko ya wananchi yanayoletwa Wizarani kwa njia ya kielektroniki,



malalamiko hayo yanaweza kuwa yanahusu masuala ya ndoa, mirathi, ardhi n.k, ili kutuma lalamiko mwananchi atalazimika kutengeneza akaunti kwa kujisajili na kujaza taarifa zote muhimu.

Wananchi wanaweza kuufikia mfumo huu kwa anuani ya; <https://smmis.sheria.go.tz/> na kufuata maelekezo.

3. MFUMO WA MAOMBI YA KUONGEZWA MUDA WA KUFUNGUA MASHAURI MAHAKAMANI (Extension Handling System)

Ni mfumo kwa ajili ya kupokea na kuchakata maombi ya kuongezwa muda wa kufungua shauri lililopita muda wa kisheria mahakamani kutokana na sababu mbalimbali.

ili kutuma maombi muwasilishaji maombi atatakiwa kujisajili kwenye mfumo kwa kujaza taarifa zote muhimu.

Aidha baada ya ombi kupokelewa mwananchi atapata mrejesho kupitia simu au barua pepe yake aliyojiza.



Wananchi na wadau wanaweza kuufikia mfumo huu kwa anuani ya; <https://smmis.sheria.go.tz/> na kufuata maelekezo.

4. MFUMO WA MAOMBI YA KUACHILIA WAFUNGWA WENYE CHANGAMOTO YA AFYA YA AKILI (Discharge Order)

Ni mfumo wa kuchakata maombi ya vibali vya kuachia wafungwa na wagonjwa wenye changamoto za afya ya akili kwenye taasisi ya Isanga iliyopo Jijini Dodoma.

Ili kutumia mfumo afisa kiungo wa Taasisi ya Isanga anayehusika na masuala hayo atatengenezwa akaunti na wasimamizi wa mfumo kutoka Wizara ya Katiba na Sheria. Aidha baada ya ombi kushughulikiwa mrejesho utatumwa kwa njia ya mfumo.

Mfumo huu unafikiwa kwa anuani: <https://smmis.sheria.go.tz/> na kufuata maelekezo yanayotolewa.



5. MFUMO WAMAOMBI YA MSAADA WA KISHERIA (Legal Aid Services)

Ni mfumo unaotumika kupokea na kuchakata maombi yanayohusu msaada wa kisheria, ili kutuma maombi ya msaada wa kisheria mwananchi atalazimika kujisajili kwa kujaza taarifa zote muhimu.

Aidha baada ya ombi kupokelewa mwananchi atapata mrejesho kupitia ujumbe mfupi kwenye simu yake au barua pepe.

Mfumo unapatikana kwa anuani ya;

<https://smmis.sheria.go.tz/>

6. MFUMO WA KUSAJILI WANASHERIA WA SERIKALI (Government Lawyers Database)

Ni mfumo wa kusajili Wanasheria wa Serikali kwa lengo la kutambua maeneo yao ya ubobezi.

Faida za mfumo huu ni kusaidia wafanya maamuzi kuwapa majukumu Wanasheria wa Serikali kulingana na maeneo yao ya ubobezi.

Mfumo huu unapatikana kwa anuani ya;-

<http://lawyers.gov.go.tz/>



7. MFUMO WA USAJILI WAWATOA HUDUMA ZA MASUALA YA UPATANISHI, MASHAURIANO, MARIDHIANO NA USULUHISHI

Ni mfumo unaohifadhi taarifa za usajili wa watoa huduma za masuala wa Upatanishi, Mashauriano, Maridhiano na Usuluhishi, Kama sheria ya Usuluhishi ya mwaka 2021 inavyoelekeza, hadi sasa kupitia mfumo watoa huduma 152 wamesajiliwa.

Aidha mfumo huu unarahisisha usajili na kuwatambua watoa huduma wa masuala hayo kwa urahisi.

Mfumo huu unapatikana kupitia anuani ya;

<https://mmuu.sheria.go.tz/>

8. MFUMO WA TAFSIRI YA KISWAHILI YA SHERIA (MTKS)

Ni mfumo unaolenga kusaidia kufanya ufuatiliaji kazi ya kutafsiri sheria kwa lugha ya Kiswahili.

Aidha, kupitia mfumo wananchi wanaweza kujua hatua iliyofikiwa katika zoezi la kutafsiri sheria kwa lugha ya Kiswahili ikiwa ni pamoja na kujua idadi ya sheria zilizotafsiriwa hadi sasa. Mfumo huu unapatikana kupitia anuani ya;

<https://mtks.sheria.go.tz/>

Mawasiliano
Wizara ya Katiba na Sheria Mji wa Serikali, Mtumba S.L.P. 315, DODOMA.

Masijala: barua@sheria.go.tz Simu: +255 26 2310021 Nukushi: 255 26 2321679
Barua pepe: km@sheria.go.tz

Twitter: @Sheria_Katiba

Instagram: @Katibanasheria_

Facebook: Wizara ya katiba na sheria


Blogu: katibasheria.blogspot.com

Tovuti: www.sheria.go.tz



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA KATIBA NA
SHERIA

MIFUMO YA KIELEKTRONIKI YA
UTOAJI WA HUDUMA ZA KISHERIA



Mfumo huu unafikiwa kwa anuani ya
<https://smmis.sheria.go.tz>